

## Utangulizi

Toba ni zaidi ya kusema tu samahani. Ni kuiacha kabisa ile dhambi tulioitenda, kumuomba Mungu msamaha na kuamua kuwa tunataka kufuata njia za Mungu pale tunapokutana na majaribu ya kutushawishi kutenda dhambi (kwa taarifa juu ya dhambi rejea Somo nambari 1). Toba ya kweli inamaana kubadilisha kabisa mitazamo ya kiakili, na kuwa na huzuni juu ya dhambi. Haya ni ‘madadiliko ya moyo’ na matendo – tendo maalum la kumuomba Mungu msamaha. Tunapokuwa na majuto na ‘kutubu’ peke yake si toba.

Bibilia inatupa mafundisho ya wazi juu ya toba la dhambi either kwa siri kibinafsi au hadharani.

## Toba ni kwa Mungu

Hii ni kutambua ya kwamba ni Mungu tunaye mtendea dhambi.

*Zaburi 32:5 – Kisha nilikiri makosa yangu kwako; wala sikuuficha uovu wangu. Nilisema ninakuung-mia makosa yangu ee Mwenyezi – Mungu, ndipo nawe ukonisamehe dhambi zangu zote.*

*Zaburi 51:4 – Nimekukosea wewe peke yako, nimetenda yaliyo mabaya mbele yako. Uamuzi wako ni wa haki, hukumu yako haina lawama.*

## Toba ni Muhimu

– Ila si lazima iwe hadharani: Ahadi ya Mungu ya kusamehe, inategemea pale ambapo kukiri inakuvwa ni sehemu ya toba (Tazama 1 Yohana 1:9).

## Toba inatolewa kwa yule aliye tendewa kosa?

– Kama inawezekana, ingawa jambo hili linapaswa kufanywa kwa uangalifu mkubwa, na pia kama huna uhakika wa jinsi ya kufanya, pata ushauri kutoka kwa rafiki wa Kikristo unayemuamini ama mchungaji (Hesabu 5:6-7).

## Toba la dhambi kwa Wakristo wengine

Yakobo alifundisha ya kwamba tunapaswa kuijungamia dhambi sisi kwa sisi (Yakobo 5:16). Yakobo alifundisha ya kwamba toba, na mara nyingine ukombozi, ni muhimu kabla ya kumsogelea Mungu (Mathayo 5:23-24). Jambo hili huonekana pale ambapo yule aliye kwazwa anafahamu ya kwamba ametendewa kosa. Kwahiyo, kama asipohisi jambo lolote, inaweza kumuumiza zaidi iwapo ataam-biwa, kwamfano kama kuna mawazo ya chuki ambayo ulikuwa nayo dhidi yake.

Mathayo 21:28-31; 27:3-5; 2 Samueli 12:13-18; Zaburi 51:10; Luka 15:17, 18, 20; Matendo 8:21-22; 2 Wakorintho 7:9-10

## Toba huja kabla ya kuzaliwa upya

(Tazama Yohana 3:1-16.)

Toba ni ufunguo unaofungua mlango ambao mtu kwa imani huingia kwenye uzima wa milele. Imani inayookoa haiwezekani bila ya toba

Mathayo 3:2, 8; 4:17; 9:13; Luka 24:47, 48; Matendo 2:38; 17:30; 20:20-21; 26:19-20

### Kutokuwa na nia ya kutubu humpofusha mtu

Na hatimaye kufanya ufahamu wake kuwa mgumu.

Mathayo 11:15, 20, 22; 1 Yohana 1:6, 8, 10; Isaya 1:13-15; Waebrania 6:6; Luka 13:3

### Mungu mara kwa mara anamuonya mtu asiyetubu

– Lakini mikono ya Mungu mara zote huwa wazi kumpokea yule anayetubu.

Ezekieli 18:31-32; 2 Wakorintho 5:20 na 6:2; Luka 15:7; 15:20; Ufunuo 2:5, 16, 21; 3:3, 19; Warumi 10:21

### Ufupisho

Toba ya kweli ni ya muhimu iwapo wanadamu wataweza kuwa na amani na Mungu. Toba ya kweli inahusu kubadilisha mtazamo wa kiakili – mabadiliko ya moyo. Mungu ni wa haki hiyo hati21

ma ya yote atahukumu dhambi. Lakini ametupatia ufumbuzi wa kudumu katika kuikabili dhambi: kafara aliyoitoa Yesu pale msalabani kwaajili ya dhambi zetu. Sisi tunapaswa kutubu ( kuziacha) dhambi zetu, tuwe na mabadiliko ya moyo yaliyo ya kweli na ya kudumu, tumuamini na kumtege-mea Yesu Kristo kama ni Bwana na Mwokozi, na ndipo tuendelee kumuamini na kutegemea.

Mungu anaahidi ya kwamba iwapo tutamuomba yeye atatujaza wake Roho Mtakatifu. Ataendelea kutusaidia wakati wowote tunapajaribiwa kutenda dhambi tena. Hili hakika ni wazo la ajabu.

Copyright © Sovereign World Trust, PO Box 777, TONBRIDGE, Kent, TN11 0ZS, UK  
[www.sovereignworldtrust.org.uk](http://www.sovereignworldtrust.org.uk)

#### Publishing and Translation History

First Published in English by Glory to Glory Publications.

Christian Publications International, PO Box 212, Saffron Walden, CB10 2UU - [www.christian-publications-int.com](http://www.christian-publications-int.com)  
Editor Peter Sammons. Contributors Alex Jacob, David M. Moore, Peter Byron- Davies, Greg Stevenson, Peter Sammons  
ISBN English 978-0-9567831-6-5

This Kiswahili translation for Sovereign World Trust by Revd John Y Madinda with permission  
Swahili Edition Published by Sovereign World Trust ISBN - Kiswahili 978-1-908010-12-4